Matumizi ya lugha za asili: Mfano wa Lugha ya Kirangi

Makala itakayotolewa katika Kumbukumbu za Kongamano la Kwanza juu ya Hali ya Lugha za Tanzania, Juni 18-19, 2004, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Oliver Stegen <oliver@ling.ed.ac.uk>

SIL	Idara ya Kiisimu
S.L.P. 1369	AFB, George Square
Dodoma	Edinburgh EH8 9LL
Tanzania	Uingereza

Muhtasari: Makala hii inachunguza nafasi zinazobaki kwa matumizi ya lugha za asili kimaandishi wakati lugha ya taifa Kiswahili hutumiwa katika maeneo mengi ya maisha ya kila siku. Lugha husika ya makala hii ni lugha ya Kirangi ambayo huongewa na wasemaji zaidi ya laki tatu katika Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma. Tangu 1996, shirika la SIL limetoa huduma ya maendeleo ya lugha ya Kirangi; hasa, wanashirika kwa msaada wa Warangi wenyewe wameunda mfumo wa herufi, yaani alfabeti ya Kirangi, pamoja na uchapishaji wa maandiko mbalimbali.

Ili kugundua Warangi wangetumia lugha yao kwa aina ya maandiko yapi, utafiti wa kiisimu-jamii ulifanyika. Wasemaji Warangi zaidi ya mia moja wameshajaza hojaji, nayo majibu yanaonyesha kwamba asilimia zaidi ya thelathini wanadai kwamba wanatumia lugha ya Kirangi kwa ajili ya kuandika, k.m. barua za binafsi. Tena, karibu nusu walisema kwamba wana hamu ya kusoma maandiko ya Kirangi kama vile hadithi za kale. Kufuatana na matokeo ya hojaji hiyo, kalenda ya mwaka 2004 imechapishwa inayoonyesha methali za Kirangi. Pia, Warangi wengine wameanza kukusanya methali nyingine na hadithi za kilugha ili kuzihifadhi kwa vizazi vijavyo.

Aidha, kuna nafasi katika idara ya elimu. Kwa vile wengi wameshaandika lugha ya Kirangi katika barua za binafsi, itafaa kuboresha matumizi hayo kwa kufundisha maandishi ya Kirangi, yaani herufi zilizoundwa rasmi. Ilivyoonyeshwa wazi na Tabouret-Keller na wengine (1997), mazoezi ya kusoma na kuandika katika lugha ya asili yataimarisha uwezo wa kusoma na kuandika katika lugha ya taifa.

1. UTANGULIZI

Mada ya makala hii ni matumizi ya lugha za asili inavyopaswa kwa kongamano hilo juu ya hali ya lugha za Tanzania. Kabla hatujaangalia lugha yetu ya mfano kwa ndani, yaani lugha ya Kirangi, lazima kueleza misingi ya uchunguzi huo. Tunasisitiza hasa vipengele sita:

Kwanza, tunadai kuwa lugha za asili hazitakufa kwa uwingi, ijapo Batibo (2000:11) amedai kinyume na madai yetu. Ingawa pia Abdulaziz (1993:423) amedokeza kwamba inawezekana lugha za asili za Tanzania zitatoweka mwisho wa karne hii ya 21, na Kiswahili kitakuwa lugha ya asili ya Watanzania wote, anaweka sharti "ikiwa sera zilizopo zitaendelea" (tafsiri yangu). Tangu mwaka wa 1997 lakini, sera za lugha zimebadilishwa rasmi; tarehe 23 Agosti 1997, Sera ya Utamaduni ilipitishwa ikisema:

> §3.2.1 Jamii zetu zitaendelea kutumia na kujivunia lugha zake za asili.
>
> §3.2.2 Wananchi, mashirika ya umma na ya watu binafsi yatahamasishwa kuandika, kukusanya, kutafiti, kuhifadhi na kutafsiri lugha za asili katika lugha nyinginezo.

Siyo kusema kuwa sera hiyo imeanzisha ufufuko wa lugha za asili, bali utambuzi wa fahari iliyohisika kuhusu lugha za asili umechangia katika kubadilishwa kwa sera. Katika jamii nyingi za Tanzania, kumetokea hali

imara ya uwili lugha, yaani lugha zote mbili - lugha ya taifa Kiswahili na lugha ya asili - hutumiwa katika maeneo tofauti. Kwa kawaida, Kiswahili kinashika nafasi ya maandishi na ya maeneo rasmi kama ofisini, shuleni n.k., na lugha ya asili hutumiwa hasa nyumbani na kwa mawasiliano ya binafsi na mambo ya utamaduni. Kadiri hayo ya pili yataelekea kutumia maandishi pia, lugha za asili zitapata fursa ya kuendelezwa kimaandishi.

Pili, matumizi ya lugha za asili hufuata mahitaji ya wasemaji wenyewe. Kwa hiyo, hatua za kuiendeleza lugha ya asili pia yafuate mahitaji ya jamii. Ndivyo anavyoeleza Carrington (1997:90) akiwashauri waalimu wa kusoma na kuandika kilugha watambue na kuyafanyia kazi maeneo yale ya maisha ya wenyeji ambayo katika yake faida ya masomo itakuwa wazi kwa wasemaji wa lugha husika. Hapo lakini, kazi ya wataalamu wa kiisimu na kazi ya waalimu wa kilugha na wengine wanaoleta maendeleo ya lugha za asili huwa hazijaenda sambamba wala kuelekea lengo moja. Blommaert (1997) anakosoa makala za kiisimu zisizo na faida kwa wasemaji wa lugha husika kwa vile zimeandikwa kupitia macho ya watu wa nje. Bila kubadilisha njia zao za kuchunguza na kutolea matokeo ya uchunguzi, wanaisimu hawataleta faida inayohitajika katika jamii ya lugha.

Tatu, huduma ya kusoma na kuandika kilugha iendelezwe kwenye mahali pa lugha husika badala ya kwenye ngazi kuu ya kitaifa. Halvorson (1970) anatoa wasifu ya huduma moja ya masomo ya kilugha Mkoani mwa Singida iliyofaulu vizuri zaidi kuliko huduma ya masomo ya Kiswahili katika maeneo yaleyale. Aidha, katika kulinganisha huduma za kusoma na kuandika katika lugha za asili kule Kenya na huduma zilezile hapa Tanzania, Fasold (1997:252) anasisitiza kuwa vijitabu vya kilugha vilivyochapishwa katika ngazi ya umma vilipokelewa vizuri zaidi kuliko vile vilivyochapishwa katika ngazi ya kitaifa.

Nne, lugha za asili zitaongeza ujuzi katika masomo mengine, hasa historia na fasihi, alivyosisitiza Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Nyerere katika hotuba zake, k.m. “Sisi hapa Tanzania tumevutwa hasa na fursa za uchunguzi wa kihistoria unaounganisha fasihi andishi na fasihi simulizi kwa vile inaonekana kama itahusika sana na kugundua tena historia yetu yenyewe” (Nyerere 1968:83, tafsiri yangu).

Tano, lugha za asili zitaendelea kutumiwa hasa katika nyimbo, hadithi, mahubiri, methali n.k., maana yake kuna sehemu muhimu za elimu zinazotegemea lugha za asili. Kwa vyovyote, lugha za asili, kama chanzo cha mawazo na mtazamo wa binadamu, huathiri mwenendo na maamuzi katika maisha ya kila siku alivyoonyesha Staewen (1991). Vivyo hivyo, Nyerere (1968:268) amesisitiza kwamba elimu ya kiafrika ilivyoendeshwa kabla ya wakati wa ukoloni isitupwe bali ikamilishe elimu ya shuleni. Basi, elimu ya asili na elimu rasmi zikamilishane badala ya kugombeana.

Sita na mwisho, uwezo wa kusoma na kuandika utaimarishwa ukifundishwa kwa lugha ya asili, au lugha ya mama. Alivyodokeza Le Page (1997:65,68), njia bora ya kupata elimu ya juu katika lugha ya kitaifa au kimataifa, ni kuanza elimu ya msingi katika lugha ya asili. Hata hivyo, wenyeji wengi hawajaamini kuwa lugha ya asili inaleta elimu bora, ingawa imeonyeshwa kitaalamu kuwa hivyo. Sasa ni jukumu la wanaisimu na walimu wa lugha kuwaridhisha Watanzania kwamba lugha za asili zina thamani na faida kielimu.

Kwa mujibu wa vipengele hivyo sita, tutaiangalia sasa lugha yetu ya mfano.

2. HALI YA KIRANGI

Lugha ya Kirangi huongewa katika Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma, na wasemaji wake sio wachache. Alivyoonyesha Legère (2002:165), siyo rahisi kuhakikisha idadi ya wasemaji wa lugha fulani ya Tanzania kwa vile katika sensa za zamani, Watanzania waliulizwa kuhusu kabila lao na siyo kuhusu lugha. Tena, tangu mwaka wa 1967 hakuna sensa iliyouliza swali hata la kabila. Tukitaka kupata idadi ya watu wanaoongea lugha ya Kirangi, tunaweza kuanza na idadi ya watu waliojiita Warangi katika sensa ya mwaka wa 1957, yaani watu 110,292 ilivyodondolewa na Polomé (1980:4). Kwa mwaka wa 2000, idadi ya Warangi imekadiriwa kuwa 310,000 (Grimes 2000). Idadi hiyo imekadiriwa kutokana na idadi ya watu kwa jumla katika Wilaya ya Kondoa waliohesabika katika sensa ya mwaka wa 1988 inavyoonyeshwa katika mstari wa pili wa jedwali ya 1 huko chini. Kuanzia mwaka wa 1997 hadi mwaka wa 1999 nimetembelea vijiji vya Warangi katika kila kata ya Wilaya ya Kondoa, na kupata makadirio ya asilimia ya Warangi wanaoishi katika kila kata inavyoonyeshwa katika mstari wa tatu na wa nne katika jedwali ya 1. Hivyo tumepata makadirio ya idadi ya Warangi ndani ya Wilaya ya Kondoa kwa mwaka wa 1988, ni watu 213,800. Tukizidisha idadi hiyo kwa asilimia 2.4, yaani kima cha ongezeko cha kila mwaka kilichopatikana kutoka maofisi ya kata za Wilaya ya Kondoa kwa miaka ya tisini, tutapata idadi ya Warangi walioishi katika Wilaya ya Kondoa mwaka wa 2000, ni Warangi 284,189. Lazima kuzingatia lakini kuwa Warangi wengi wanakaa nje ya Wilaya ya Kondoa, na kuna

majumuia makubwa ya Warangi katika wilaya za Babati, Kiteto, na Dodoma Vijijini, na pia katika miji ya Arusha, Tanga, Dar es Salaam, Morogoro, na Dodoma, kutaja yale yenye umuhimu wa kwanza tu. Tumekadiria kuwa asilimia kumi za Warangi wangeweza kukaa nje ya Wilaya ya Kondoa. Hivyo, idadi ya Warangi kwa jumla mwaka wa 2000 ingefika watu 312,608. Kulingana na idadi hiyo, kuna vipengele viwili ambavyo vingeathiri idadi ya wasemaji wa lugha ya Kirangi: Kwanza, kuna wale Warangi wanaoongea Kiswahili kama lugha yao ya kwanza; pili, kuna watu wa makabila majirani, kama Wasi (wanaoitwa pia Waalagwa) au Waburunge wanaoongea Kirangi kama lugha yao ya kwanza. Kwa bahati mbaya hakuna uchunguzi wa kuhamisha lugha katika Wilaya ya Kondoa. Hata hivyo, tumekadiria idadi ya wasemaji wa lugha ya Kirangi ikaribie idadi ya Warangi, hasa kwa vile hatujamkuta Mrangi asiyeweza kuongea lugha ya Kirangi. Kwa vyovyote, iko wazi kwamba lugha ya Kirangi imekua katika nusu karne iliyopita, na haimo katika hatari ya kutoweka mapema.

Jedwali ya 1: Idadi ya Warangi katika Wilaya ya Kondoa

Jina la Kata	Idadi ya Watu 1988	Makadirio ya Asilimia ya Warangi	Idadi ya Warangi 1988
Bereko	12,445	70	8,700
Kikilo	7,679	50	3,800
Kisese	16,964	80	13,500
Masange	11,133	95	10,500
Mnenia	9,907	95	9,400
Chandama	15,691	80	12,500
Chemba	7,821	70	5,400
Goima	15,318	50	7,600
Mrijo	7,822	60	4,700
Kolo	7,646	80	6,100
Soera	5,799	30	1,700
Changaa	9,585	40	3,800
Thawi	9,570	15	1,400
Kingale	9,328	90	8,400
Kondoa Mjini	19,511	60	11,700
Suruke	8,342	75	6,200
Dalai	11,020	70	7,700
Jangalo	15,546	85	13,200
Mondo	8,656	75	6,500
Paranga	11,389	70	7,900
Bumbuta	9,654	95	9,100
Busi	11,640	90	10,400
Haubi	11,007	99	10,900
Kalamba	11,975	99	11,800
Kwadelo	7,104	85	6,000
Pahi	15,711	95	14,900
Jumla/Wastani	**288,263**	**74**	**213,800**

Chini ya vichwa vidogo vifuatavyo tutaeleza mahusiano kati ya uchunguzi wa kiisimu na matumizi ya lugha, na mwishowe tutapendekeza hatua za kufanya kulingana na hali ya lugha.

2.1 Uchunguzi wa Kiisimu Uliofanyika

Tunaweza kugundua nyakati mbili hasa za kuichunguza lugha ya Kirangi kiisimu. Makala za kwanza zilitolewa wakati wa utawala wa Wajerumani, kama Seidel (1898) anayeandika sarufi fupi pamoja na msamiati wa maneno 800 na sentensi 114, na Dempwolff (1916) anayetoa wasifu ya fonolojia hasa, pamoja na pendekezo la mfumo wa herufi. Baada ya hapo hakuna makala ya kiisimu nyingine karibu kwa karne nzima. Makala ya karibuni zaidi ni hizi za Akhavan (1990) anayechanganua hadithi moja ya Kirangi kimofolojia na kisintaksia akizingatia hasa vidatu lafudhi, Dunham (2001) anayetoa wasifu ya fonolojia, mofolojia na sintaksi pamoja na msamiati wa maneno 1,600 ya Kirangi na tafsiri zake kwa Kifaransa na Kiingereza, na Stegen (2002) anayetoa wasifu ya unyambuaji wa nomino na vitenzi pamoja na kifupisho cha fonolojia na mofolojia. Makala hizo zote zimeandikwa katika lugha za kigeni, yaani Kijerumani, Kifaransa na Kiingereza, tena zimeandikwa kufuatana na nadharia ya kiisimu zikitumia istilahi ya kiisimu. Kwa hiyo, Warangi kwa jumla

hawajafaidika na aina hiyo ya uchunguzi wa kiisimu. Inafaa kukumbuka kwamba, nje ya kazi ya SIL, hasa Bergman na wengine (1996) na Stegen (2004), hakuna uchunguzi wa kiisimu-jamii miongoni mwa Warangi.

Kwa njia nyingine, wanashirika wa SIL wamejaribu kuwahamasisha Warangi wahudhurie katika maendeleo ya lugha yao. Njia hii imeelezwa kinadharia na Kutsch Lojenga (1996). Utekelezaji wa njia hiyo katika huduma ya lugha ya Kirangi ulisababisha mkutano ulioanzishwa na Warangi wenyewe, tarehe 6 Oktoba 1998, ambapo wawakilishi zaidi ya 30 walikubaliana kuhusu jinsi ya kuandika lugha yao ya Kirangi. Kuanzia Februari 1999 hadi Januari 2000, kamati ya maendeleo ya lugha ya Kirangi (MALUKI) ilifanya kazi. Tena, semina ya siku nne kuhusu kusoma, kuandika, kutunga kamusi, na kutafsiri ilifanyika Mei 1-4, 2002, nao wenyeji waliohudhuria walikuwa zaidi ya 40. Kufuatana na semina hiyo, kamati ya lugha yenye Warangi sita waliojitolea ilianza kufanya kazi kutoka Mei 2002 hadi Juni 2004. Matokeo ya kazi ya wanakamati, yaani Warangi wenyewe kwa msaada wa shirika la SIL, ni uchapishaji wa maandiko ya kilugha yafuatayo: Kijitabu cha masomo ya awali (Oktoba 1999), mifano halisi mitatu kutoka Injili ya Luka (toleo la kwanza Julai 2000, toleo la pili Machi 2004), jedwali ya alfabeti (toleo la kwanza Aprili 2001, toleo la pili Februari 2004), kipeperushi cha herufi za Kirangi (Novemba 2003), kalenda yenye methali za Kirangi (Januari 2004), na kipeperushi cha Zaburi 23 (Mei 2004). Matokeo hayo yote yamepokelewa na wenyeji vizuri tu, nao wamefurahi kuona lugha yao kimaandishi na kukumbushwa mambo ya lugha kama methali ambayo yameshaanza kusahauliwa na wengine.

2.2 Matumizi ya Lugha ya Kirangi katika Jamii

Asilimia kubwa ya Warangi ni wakulima wanaoishi vijijini huku wilayani mwa Kondoa. Wengine, hasa katika miji ya Kondoa, Bereko na Pahi, wanajishughulikia na biashara ya mazao na bidhaa mbalimbali. Kuna dalili zinazoonyesha kuwa lugha ya Kirangi hutumiwa sana, siyo nyumbani tu lakini pia masokoni. Zaidi ya hayo, matumizi ya Kirangi yameangaliwa mahali pafuatapo: mapambio ya kanisani, mikanda ya muziki, wito ulioandikwa kwenye teksi na basi, na salamu katika barua za binafsi. Ni wazi kuwa Kiswahili hutumiwa katika huduma za umma. Ili kugundua matumizi ya lugha ya Kirangi kitaalamu, uchunguzi wa kiisimu-jamii ulifanyika kwa kutumia hojaji (angalia kiambatisho). Watu 113 walijibu hojaji, wakiwakilisha wanaume na wanawake, wanamji na wanakijiji, wenye elimu na wasioelimika, wazee na vijana. Matokeo mengine ya uchunguzi huo yanayohusu matumizi ya maandishi hasa yametolewa katika Stegen (2004). Kwa jumla, tunaweza kutoa taarifa ya mitazamo ifuatayo:

- Asilimia 33.3 za waliojibu wamedai kutumia lugha ya Kirangi kimaandishi mara kwa mara. Matokeo hayo hayategemei umri; katika rika la chini ya miaka 35 ni asilimia 34.8, rika la 35-55 ni asilimia 32.2, na rika la juu ya 55 ni asilimia 32.2.
- Karibu wote (asilimia 96.2) huandika barua za binafsi (hakuna aina nyingine ya maandiko ambayo yangetumiwa zaidi ya barua); baina yao, asilimia 19.2 hutumia lugha ya Kirangi. Asilimia 26.5 za ziada wamesema kwamba wangependa kuandika barua kwa Kirangi lakini hawajaweza.
- Matakwa ya Warangi upande wa maandiko ya Kirangi ni maandiko ya kidini (asilimia 55.7), historia ya Warangi (asilimia 49.5), hadithi za asili (asilimia 45.1), na kamusi (asilimia 22.1). Maandiko mengine hayakutajwa mara nyingi kama hayo.

Matokeo hayo yanadokeza kuwa Warangi wenyewe wameanza kutumia lugha yao ya asili hata katika maeneo ya kimaandishi, na wamegundua mahitaji ya kuendeleza lugha ya Kirangi kwa matumizi ya binafsi. Kulingana na mapendekezo na matakwa ya wenyeji wenyewe, itafaa kubadilisha njia na mwelekeo wa huduma ya maendeleo ya lugha ya Kirangi. Hasa mafundisho ya kuandika barua na uchapishaji wa historia na hadithi yatunzwe vizuri zaidi.

2.3 Mapendekezo kwa Hatua Zijazo

Tukizingatia uchunguzi ulioelezwa hapo juu, tunaweza kupendekeza utendaji wa aina mbalimbali utakaofaa katika kuboresha na kusaidia matumizi ya lugha ya Kirangi kwa mujibu wa matakwa ya Warangi wenyewe.

Kwanza, wasifu ya lugha ya Kirangi ipatikane ambayo itaeleweka kwa wenyeji; maana yake, iandikwe kwa Kiswahili na isitumie istilahi ya hali ya juu.

Pili, kulingana na matakwa ya Warangi, hadithi za asili zikusanywe na kuchapishwa katika vijitabu. Tena, historia ya Warangi iandikwe kufuatana na kumbukumbu za wazee. Wakati uleule, na kamusi itolewe, ikiwezekana iwe na lugha tatu: Kirangi-Kiswahili-Kiingereza ili kurahisisha upatikanaji wa elimu ya juu.

Tatu, kwa vile theluthi moja ya Warangi wameshaanza kutumia lugha ya Kirangi kimaandishi, hasa katika kuandika barua za binafsi, na wengi zaidi wangependa kuitumia hivi, itafaa kuendesha semina ya kuandika barua za kilugha, pamoja na kufundisha matumizi ya herufi rasmi, mpangilio wa barua, na kanuni za uandishi bora. Ikiwezekana mafundisho hayo yaendelezwe katika ushirikiano na idara ya elimu ya watu wazima.

Nne na mwisho, masomo ya darasa la kwanza yaendelezwe katika lugha ya Kirangi kwa matumizi katika maeneo ya vijijini ambapo lugha ya asili hutumiwa peke yake. Watoto wa darasa la kwanza wakipata kusoma, kuandika na kuhesabu kupitia lugha ya asili wakati Kiswahili ni somo la kila siku, wataelewa rahisi zaidi na kutekeleza masomo yao hata katika lugha ya taifa kuanzia darasa la pili. Hatua hiyo lakini, lazima kuijadili na idara ya elimu kwanza na kushirikiana na wakuza mitalaa.

3. HITIMISHO

Katika makala hii ni matumaini yetu ya kwamba tumeonyesha wazi mambo matatu:

1. Ilivyotambulika katika Sera ya Utamaduni ya 1997, wenyeji wa Tanzania wataendelea kutumia na kujivunia lugha za asili.
2. Ilivyoonyeshwa na Tabouret-Keller na wengine (1997), wenyeji watafaidika kupata elimu bora katika lugha ya taifa wakijifunza kusoma na kuandika katika lugha yao ya asili.
3. Uchunguzi wa kiisimu na hasa wa kiisimu-jamii unaweza kuchangia mengi katika maendeleo ya lugha za asili. Kufuatana na matokeo ya uchunguzi huo, kutakuwa na nafasi nyingi za kuleta mafundisho na maandiko ya kilugha yanayohitajika kwenye ngazi ya umma.

Maendeleo ya lugha za asili yakitekelezwa kwa kuzingatia kilichogunduliwa katika uchunguzi, faida zitakuwa nyingi, katika elimu, katika fasihi, katika historia, na nyinginezo.

Shukrani

Uchunguzi huo umewezeshwa kupitia kibali cha kukaa nchini Tanzania, namba C 021903. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Kanisa la Anglikana, Dayosisi ya Kondoa, ambao wameandika barua ya mwaliko ili nipate kibali hicho. Kwa misaada mbalimbali, nawashukuru Dk. Assibi Amidu, Prof. Karsten Legère, Andrew Lujuo, Mch. George Mwita, Peter Patrick, na Dorothea Stegen. Ikiwa kuna upungufu au kasoro yoyote iliyojitokeza katika makala hii, nakiri kwamba sio waliotajwa hapo juu hawahusiki, bali mimi binafsi ndiye ninahusika na upungufu huo.

Marejeo

Abdulaziz, Mohamed. 1993. “Language use and language development: Review of sociolinguistics theory”, katika: Foley, William (mhariri). *The Role of Theory in Language Description*, Berlin/New York: Mouton de Gruyter, uk. 421-436.

Akhavan, Firouzeh. 1990. “Untersuchungen zur Grammatik des Irangi anhand des Materials aus dem Nachlass Dr. Paul Berger”, Tasnifu ya Shahada ya Pili, Chuo Kikuu cha Hamburg, Ujerumani.

Batibo, Herman. 2000. “The Linguistic Situation of Tanzania”, katika: Kahigi, Kulikoyela, Yared Kihore & Maarten Mous (wahariri). *Lugha za Tanzania - Languages of Tanzania*, CNWS Publication 89, Chuo Kikuu cha Leiden, Uholanzi, uk. 5-17.

Bergman, Ted, Joseph Mbongué, Rachel Sowers & Tracy Tooley. 1996. “Sociolinguistic Survey among the Rangi (Langi)”, Muswada usiotolewa rasmi, Dodoma: SIL.

Blommaert, Jan. 1997. *State Ideology and Language: The Politics of Swahili in Tanzania*. LICCA Papers 3, Duisburg: Chuo Kikuu cha Gerhard Mercator, Ujerumani. Imepatikana kutoka http://africana.rug.ac.be/texts/research-publications/publications_on-line/Swahili_in_Tanzania.htm

Carrington, Lawrence. 1997. “Social Contexts Conducive to the Vernacularization of Literacy”, katika: Tabouret-Keller na wengine, uk. 82-92.

Dempwolff, Otto. 1916. “Beiträge zur Kenntnis der Sprachen in Deutsch-Ostafrika - 8. Irangi”, *Zeitschrift für Kolonialsprachen* 6, Berlin, uk. 102-123.

Dunham, Margaret. 2001. “Description ethno-linguistique des Valangi de Tanzanie”, Tasnifu ya Shahada ya Udaktari, Chuo Kikuu III cha Paris, Ufaransa.

Fasold, Ralph. 1997. “Motivations and Attitudes Influencing Vernacular Literacy: Four African Assessments”, katika: Tabouret-Keller na wengine, uk. 246-270.

Grimes, Barbara (mhariri). 2000. *Ethnologue - Languages of the World*, Toleo la Kumi na Nne, Dallas: Summer Institute of Linguistics.

Halvorson, Marian. 1970. “An adult literacy program: Central Tanzania 1955–1968”, *Notes on Literacy* 9, Dallas: Summer Institute of Linguistics, uk.1-15.

Legère, Karsten. 2002. “The ‘Languages of Tanzania’ project: background, resources and perspectives”, *Africa & Asia* 2, Göteborg: Department of Oriental and African Languages, uk. 163-186.

Le Page, Robert. 1997. “Political and Economic Aspects of Vernacular Literacy”, katika: Tabouret-Keller na wengine, uk. 23-81.

Kutsch Lojenga, Constance. 1996. “Participatory research in linguistics”, *Notes on Linguistics* 73, Dallas: Summer Institute of Linguistics, uk. 13-27.

Nyerere, Julius. 1968. *Freedom and Socialism - A selection from writings and speeches 1965-1967*, Dar es Salaam: Oxford University Press.

Polomé, Edgar. 1980. “The languages of Tanzania”, katika: Polomé, Edgar & C.P.Hill (wahariri). *Language in Tanzania*, Oxford University Press, uk. 3-25.

Seidel, Alfred. 1898. “Grammatik der Sprache von Irangi”, katika: Werther, Waldemar (mhariri). *Die mittleren Hochländer des nördlichen Deutsch-Ost-Afrika*, Berlin, uk. 387-434.

Staewen, Christoph. 1991. *Kulturelle und psychologische Bedingungen der Zusammenarbeit mit Afrikanern*, Afrika-Studien 120. München: Weltforum-Verlag.

Stegen, Oliver. 2002. “Derivational Processes in Rangi”, *Studies in African Linguistics* 31(1/2), uk. 129-153.

-----. 2004. “A pilot study of writing in Rangi society”, *Edinburgh Working Papers in Applied Linguistics* 13, Edinburgh: Chuo Kikuu, uk. 102-111. Inapatikana kutoka http://www.ling.ed.ac.uk/~oliver/04ewpal.pdf

Tabouret-Keller, Andrée, Robert Le Page, Penelope Gardner-Chloros & Gabrielle Varro (wahariri). 1997. *Vernacular Literacy: A Re-Evaluation*, Oxford Studies in Anthropological Linguistics 13, Oxford: Clarendon Press.

Wizara ya Elimu na Utamaduni. 1997. *Sera ya Utamaduni*, Dar es Salaam.

Kiambatisho

Hojaji hii ya hapo chini imetumika katika uchunguzi wa kiisimu-jamii baina ya Warangi, na kutolewa katika Stegen (2004).

Jinsia yako	
Umezaliwa mwaka gani?	
Umezaliwa katika kijiji au mji gani?	
Mahali pa kuzaliwa kwa mamako	
Mahali pa kuzaliwa kwa babako	
Ukoo wako wa Kirangi	
Lugha zako za kwanza ni zipi? Umeanza kujifunza Kirangi, Chasi, Kiburunge n.k. lini?	
Umeanza kujifunza Kiswahili lini?	
Umeanza kujifunza Kiingereza lini?	
Shule ya msingi uliyoihudhuria	
Shule ya sekondari uliyoihudhuria	
Chuo chochote ulichokihudhuria	
Umewahi kuandika chochote kwa Kirangi?	
Kwa kawaida unaandika lugha gani?	
Wewe huandika barua kwa lugha zipi?	
Umewahi kuandika mashairi? Ya lugha gani?	
Umewahi kuandika nyimbo? Kwa lugha zipi?	
Umewahi kuandika hadithi? Kwa lugha zipi?	
Umewahi kuandika shajara? Kwa lugha zipi?	
Umewahi kuandika mapishi? Maelekezo mengine? Kwa lugha zipi?	
Umewahi kuandika orodha ya uwekaji hesabu?	
Umewahi kuandika kitu kingine ambacho hakijatajwa?	
Katika maoni yako, aina zipi za maandiko zingefaa kuandikwa kwa lugha ya Kirangi?	
Umewahi kuwa na hamu ya kuandika kitu fulani kwa lugha ya Kirangi na kushindwa?	
Katika maoni yako, Kirangi kina umuhimu kwa mambo gani? Eleza sababu yake.	
Katika maoni yako, Kiswahili kina umuhimu kwa mambo gani? Eleza sababu yake.	
Katika maoni yako, Kiingereza kina umuhimu kwa mambo gani? Eleza sababu.	
Je, ungenunua vitabu vya Kirangi? Vitabu vya aina gani?	
Kama una maoni mengine kuhusu lugha ya Kirangi, uyaandike: (Tumia nyuma ya karatasi pasipotosha hapa.)	